

UJUZI WA WATOTO/VIJANA KATIKA SIMULIZI ZA MAISHA

ULRICH SCHULZ-BURGDORF

Kutoka elimu ya lugha tunajua kwamba kila mtu aliyenena ana ujuzi maalum - kama *John Lyons* alivyoeleza katika kitabu chake *Language and Linguistics* (1981), katika sura kuhusu lugha na utamaduni wa wasemaji.

Lyons anatueleza kwamba kila mtu hushika ujuzi huo kwa njia ya kufunzwa lugha na huutumia ujuzi, huuongeza na huubadilisha kwa muda wa maisha yake yote ; ni jinsi yake ya kujua mambo ya ulimwengu.

Katika maelezo yafuatayo napenda kuonyesha ujuzi uliomo katika habari nilizopewa na kijana, jina lake ni Timothy Lawrence ambaye alikuwa na umri wa kumi na tatu siku zile. Ujuzi wake ni juu ya maisha yake ya kipokomo na pia ni ujuzi wa kumweleza mgeni mambo hayo - yaani ujuzi au uwezo wa kuzisimulia habari hizo. Kijana huyu alialikwa kukaa kwa muda na wanafunzi wa kijerumani wa masomo ya bidii huko Kenya, mwaka wa 1988.

Baada ya kuzungumza juu ya mambo mbalimbali ya Kenya na Ujerumani, kwa mfano ukulima, matumizi ya dawa ya kuuwa wadudu, uvuvi n.k., nimemwomba Timothy aniandikie kidogo juu ya maisha yake. Na siku moja alinipa kurasa saba zenye jina "*Maisha yangu kwa jumla*" na zilizomo habari nyingi ambazo yeye anafikiri ni muhimu zitajwe na nijulishwe.

Timothy Lawrence alijijulisha kuwa mmalanchini, yaani mpokomo kutoka sehemu ya kusini ya mto wa Tana baina ya mahali mto unapoingia baharini na mji wa Ngao. Siku zile alikuwa mwanafunzi wa Rueben Mwewe Boarding School pale Upokomo. Habari zake zinatonyesha vizuri simulizi ya maisha ya binafsi (au *autobiographical narrative*) ni nini, yenye ujuzi gani na jinsi gani ya kutazama maisha kwa macho ya mwenyeji kijana.

Hizi ni sura mbalimbali zionyeshe mtindo wake wa kusimulia - chaguo langu ya maneno ya Timothy Lawrence mwenyewe sasa:

Maisha yangu kwa jumla[:]

Kwa kweli mimi ni mwanakenya na nimepata bahati ya kuja duniani mwaka wa 1975 (...) [S]iwezi kusema kwa jinsi gani niliishi, hadi mwaka wa '78 ndipo nikaanza kuwa mjasiri wa kujua mambo. Nilipokuwa na umri wa miaka sita (6) nilikuwa napenda sana kusafiri na kuona mengi (...) ijapo sikupata Bahati kama hiyo, ilinibidi bado kutumaini kuhusu safari kama hiyo (...) [N]ikatimiza umri wa miaka saba (7), mwaka huu ndiyo ambao niliendelea kufungua macho zaidi na kuona mengi sana (...) [N]ilipokuwa darasa la tano (5) hali ikizidi kuwa nzuri na hapo ndipo nilipogutukia masomo (...)

Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na moja nikazidi kuwa na akili ya kilimo, Wakubwa zangu walinifunza jinsi ya kulima mahindi,pojo,kunde,maharagwe, mpunga, hata jinsi ya kukata mgomba (...) na mkungu mwenyewe. Kazi hizi zote nazipenda lakini mahindi na mpunga hunikasirisha sana. Hii ni kwa sababu (...) inahitajika kulinda ndege, mayonda, nguruwe, na panya (...)

[Uk. 2] Ukiona ndege sasa inakubidi uwafukuze kwani wakiingia shambani (...) kutumai kupata mpunga[.] hasa kulinda ndege mimi sipendi (...) Mahindi nayo yanahitaji kupaliliwa kwani bila kupaliliwa hufa na hupati mazao yo yote, hii ni mojawapo wa kazi ambayo nimeichukia. Baada ya yote kuwa na kazi moja ambayo vilevile ni ngumu, nayo ni kuvuna (...).

[Uk. 3&4] Singependelea sana kuongezea bali ukiangalia mwenyewe ni njia ndefu na tunapata shida sana hata hivyo tumezoea kulima (...). [P]ia tunalima ndizi kwa wingi sana (...) [H]asara tunaipata kwani kuna wanyama wa porini kama (...) nyati, ndovu, nguruwe n.k. (...) [.] nyati akiingia kwa migomba [.] hasara yake ni kuvunjavunja mimea yote ile anayoikula mpaka atakapotosheka (...) mwenye shamba (...) itambidi angoje msimu mwingine ili apate ndizi (...) [N]guruwe (...) yeye hutaka kupata ule mkungu wenyewe na anakula na kuvuruga (...) [N]dovu (...) ni mnyama hatari, mpole lakini ana tabia mbaya kwani yeye hutumia migomba kama miwa yake na hivyo sisi wakulima kwa jumla tumechoshwa sana na (...) mnyama huyu na hatumpendi sana (...) [S]isi wapokomo kwenda kushika samaki mtoni, ziwani ... [h]ali hii pia ni mojawapo ya maisha yetu jinsi ile [Uk. 5] sisi wapokomo tunaishi (...) tunapenda samaki sana na ni mojawapo ya vyakula vyetu tuvipendavyo(...).

[T]una Kamongo [kwa] Kiswahili [.] Mudfish [katika] kiingereza (...) ndiyo watu wengi wanaipenda na hata waingereza wakija [.] hula samaki hiyo(...). [T]una Mtonzi (...) [.] samaki za aina hii zina meno manne na huuma ukitia kidole ndani ya mdomo wake (...) sisi huzitumia kwa mboga yetu (...).

Mto ambao tunapenda kuogelea ni mto Tana ambao ni mpana sana. Pia maziwa ni kwa mfano: Chamadho, Jange, Kibwala cha myeuko, Girithu n.k. Hayo ni majina ya Kipokomo ambayo kila jina lina maana maalum ya kitu fulani, sijamwuliza babu yangu maana yake kwani sijafikia umri wa kujua maana yake.

[Uk. 6] Kufikia hapo [.] nadhani nimetoa taarifa ya kutosha kuhusiana na maisha ya kijiji chetu. Hivi sasa nasoma darasa la nan(...) na mwaka huu wa 1988 mwalimu wangu mkuu Mr. TOLA N. DADDAH alinichagua kuwa head prefect tarehe 8 Januari nami nilifurahi na nazidi kufurahi (...).

Mwaka huu wa '88 mwezi wa Agosti tarehe 12 (...) [n]dipo hali yangu ilibadilika, sikuwa nikihudhuria masomo ya kujisomea vizuri, nilikuwa mgonjwa. Nilienda kwa Dispensary ya mission na waliniambia ninahitaji X-Ray kwani roho yangu ilikuwa haipigi vizuri. Basi nikazidi kuvumilia na Shule zikafunguliwa, lakini sikuweza kusoma vizuri, ilinibidi niende kwa hiyo X-Ray Mombasa, ilikuwa hivi, nikiondoka nyumbani [*] (...) saa kumi na moja (...) na kufika malindi saa nne (...).

[*] nishukie EDEN ROCK HOTEL nimpate ndugu yangu, anipeleke mombasa (...).

Nilikuwa mgeni na kwa hivyo ilinibibi nitafute hoteli Eden Rock, nilifaulu mwishowe (...) lakini nikaambiwa amekwenda Mombasa kwa leave yake [S]asa nilifikiria sana, [n]jiende Mombasa nisikokujua au nikarudi T[ana] River? Nikaamua kwenda Tana River, hata hivyo sikukuwa na nauli ya [Uk. 7] kurudia. Katika hali ya kutafuta msaada nilituwakiwa kumpata mjerumani wa kike kwa jina Anne Schwa[r]tz na alinisaidia na nauli [.] pia alinipa Chakula cha Mchana kwani nilikuwa sijapata chakula.

Tulizungumza sana na ilifika saa nane mchana na ikanibidi kwenda stage ili nipate Basi ya saa tisa, Mimi ni mtu wa Bahati mbaya sana kwani nilipokwenda, ilikuwa imekwisha ondoka kitambo, shida nyingine ilinikabili, sikuwa na mahali pa kulala. Nilisumbuka sana (...) mwishowe niliamua kumuona Anne Schwa[r]tz katika Lutheran Guest House Malindi.

Ilikuwa saa moja na madakika na bahati niliruhusiwa (...) tukasalimiana nikamweleza shida iliyonikabili [.] naye akaniambia nimsubiri. Punde akaja na mtu mw[e]ngine mkubwa mwenye upana wa kadiri na mrefu. Nilimweleza mtu huyu shida yangu, kwanza

aliniuliza jina, mahali ninapoishi nami nikamjibu [;] alizidi kunistaajabisha kwa kunisalimia kipokomo. Sikusita[,] nilimjibu na akanijulisha jina lake kama Thomas Geider na kwamba alifahamiana na Babu zangu kina Joseph Mbizi, Erastus Buko (...) nami nilifurahi kwamba aliwafahamu.

Nilialikwa kwa chakula cha jioni nami nilikitumia na huku tunaongea, [w]alimieleza kwamba wao ni wajerumani ishirini waliokuja kujifunza kiswahili na kwamba watarudi kwao baada ya wiki mbili. Waliniandaka mahala pa malazi chumba nambari 4 nikalala hadi asubuhi.

Kuna mengi katika yaliyomo ambayo inawezekana kuyachambua. Hapa mimi nataja machache tu - kwa mfano: matumizi ya maneno ya Kiingereza kama *Dispensary ya mission* badala ya *duka ya dawa ya misheni*; *head prefect* kwa *mkuu wa wanafunzi*; *leave yake* kwa *likizo*; na *stage* badala ya *kituo cha basi*. Pia ni jambo la kuvutia kutazama matumizi ya harufi kubwa ambazo zipo mwanzoni mwa neno tu au neno kamili - kama katika maneno ya miji ya m/Mombasa na m/Malindi; au katika jina la mwalimu mkuu aliyeitwa Mr. TOLA N. DADDAH (- harufi kubwa zote) na pia katika maneno ya WAKATOLIKI na WAMALANCHINI ambayo hayakutajwa hapa; na baadaye katika EDEN ROCK HOTEL huko Malindi. Nafikiri kuandika kwa harufi kubwa anafanya kwa kutia mkazo; namna hii anaonyesha mambo au watu gani ni muhimu kwake. Lakini sitaingia katika mambo kama hayo sasa.

Badala ya hayo, napenda kueleza kwa kifupi namna gani insha hiyo inawezekana kuchambuliwa kwa msimamo wa elimu ya kusimulia (*narratology*): Ya kwanza napenda kutaja taratibu au mpango wa insha yake yaani kama mimi ninavyoufahamu: Mwandishi anatoa habari kuhusu miaka ya maisha yake na matokeo muhimu yao ambayo yeye aweza kuyakumbuka, pia anasimulia yaliyomo ya matokeo hayo. Inawezekana kuigawanya insha kamili katika sehemu tatu kama hizi:

Sehemu ya kwanza ni kutoka ukurasa wa kwanza mpaka ukarasa wa tano - habari za utoto mpaka umri wake wa kumi na moja zinatolewa: Mahali pa mambo hayo ni mahahli au maeneo yake pa asili Upokomo na mambo muhimu yasimuliwa ni kufanya kazi ya kulima na kwenda shule.

Sehemu ya pili ni ukurasa wa sita; mwandishi anakupa habari za miezi ya Agosti mpaka Septemba wa mwaka wa themanini na nane - wakati wa mkutano wake na kundi la wanafunzi wajerumani, muda mfupi uliopita kabla ya mkutano na muda wa mkutano wenyewe. Mahali pa mambo hayo sasa ni Upokomo na mji wa Malindi - mwandishi ataja safari yake ya kwanza kuvuka mipaka ya Upokomo na kuingia ugenini katika mji mkubwa zaidi kuliko makao yake ya asili (- Malindi pia ni mahali pa mkutano).

Sehemu ya tatu ni ukurasa wa saba (wa mwisho): Mahali ni mji wa Malindi na mji wa Mombasa, mtaa wa Likoni. Mambo ambayo yasimuliwa ni kuwa mgeni katika mji asioujua na hali ya kuhitaji msaada, shida ya kuendelea safari yake kufika Malindi bila fedha ya kutosha; lengo la safari hii ni kutazamwa na daktari wa Coast General Hospital huko Mombasa. Kwa jumla, nafikiri, inasemekana matokeo ya safiri yake ya kwanza na kukutana na wageni ambao wanamsaidia ni mada maalum katika sehemu ya pili na ya tatu.

Katika kazi yangu natumia insha hii kwa kutambua mambo mbalimbali:

Ya kwanza: tokeo la maradhi yake *roho ilikuwa haipigi vizuri*, njia gani jambo hilo linaathiri maisha yake, yaani kutoweza kwenda shule na kusoma. Na ya pili: kule kutafuta msaada wa hospitali ambayo ni *quest for therapy* kwa msimamo wa *Medical Anthropology*. Juu ya hayo katika insha ya Timothy Lawrence kimo kisa (*incident*) maalum ambacho ni ya kuvutia sana: inaonyeshwa kwa matumizi ya tarehe na taratibu maalum ya wakati mwandishi anayapa matokeo ambayo anaanza na kushikwa na ugonjwa: Kila tokeo ambalo muhimu linapewa tarehe, yaani mwaka, mwezi, siku na pengine hata saa zake. Kwa mfano kupewa cheo cha *head prefect*, mwanzo wa kusikia na kujua kuwa mgonjwa, safari kufika Malindi kwa basi na mkutano na kundi la kijerumani.

Katika mada ya "mkutano" mambo mawili yanahusiana kwa njia ya "bahati" Dhana ile inatumiwa kwa matokeo katika wakati ambao ni mzuri au mbaya - kama katika maneno ya Kiingereza *good chance* na *bad luck* au katika *mere chance* ('*contingency*') au katika Kijerumani *Zufall* "Bahati" ni matokeo au mambo ambayo kwa mtu mwenyewe haiwezekani kuyapanga - kama katika dhana ya kidini *amri ya Mungu*. Katika matokeo ya Timothy Lawrence ni bahati nzuri na bahati mbaya; yeye mwenyewe asema kuwa ni mtu wa bahati mbaya katika kukosa kupata basi na kutokuwa na nauli, chakula na mahali pa malazi ugenini. Lakini pia anataja bahati nzuri ya kukutana na rafiki wanya kutoka ugenini kwengine ambao walimsaidia.

Na pia bahati nzuri inahusika jambo ambalo ni aina ya mwujiza au ya kumstaajibisha. Jambo hilo ni kwamba mgeni aliye ni Thomas Geider si mgeni kamili au kabisa kwa sababu yeye anamjua babu wa Timothy Lawrence na anamsalimia kwa kipokomo. Na baadaye wageni wajerumani wawili walimwalika na kumpa nafasi ya kulala - wakiwa rafiki ambao hakujuana nao kwa muda mrefu sana.

Labda inasemekana kwamba mambo hayo yanampa Timothy Lawrence ujuzi mpya kwa njia ya bahati katika safari yake ya kwanza. Ugenini au dunia isiyojulikana, matokeo yake si mabaya tu au mambo ya kusumbua tu. Kwa bahati nzuri, pia inawezekana kushinda shida - ikiwa mtu hasiti kusimulia akampa mwengine habari zake.

Hatimaye, napenda kumaliza mawazo yangu kwa njia ya kuuliza swali kuhusu insha hiyo: Je, insha hiyo ni simulizi au ni fasihi? Na ikiwa ni fasihi kwa sababu imeandikwa, ni fasihi ya aina gani? Nafikiri siyo rahisi kuyajibu! Nimesema kwamba mwanzo ilikuwa mawasiliano: Timothy Lawrence nami tulizungumza juu ya mambo, baadhi yao yeye ameniandikia baadaye.

Je, Timothy Lawrence angeniambia maisha yake kwa kunena, kwa mdomo, angenipa habari ambazo hizi hizi? Au labda kusimulia juu ya maisha *kwa jumla* (!) haiwezekani namna hii? Inawezekana kwamba kutoa habari za maisha yote na kuziweka katika taratibu ya wakati kwa msaada wa ukumbusho, lazima kuziandika? Uhusiano gani baina ya ujuzi, ukumbusho na kuandika?

Timothy Lawrence

①

Utangulizi:-


Maisha yangu kioa jumla

Kwa kweli mimi ni mwanakenya na nimepata bahati ya kuja duniani mwaka wa 1975 yaani nilirafikiwa mwaka huo kwa kweli siwezi kusema kwa jinsi gani niliishi, hadi mwaka wa sabini na nani ndipo nikaanza kuwa mjasiri wa kupua mambo. Nilipokuwa na umri wa miaka sita (6) nilikuwa napenda sana kusafiri na kuona mengi na nilipenda sana kusafiri ijapo sikupata bahati kama hiyo, ilimbidi bado kutea moini kuhusu safari kama hiyo.

Miaka ikaeendelea nami nikazidi kukua hadi nikatimiza umri wa miaka saba (7), mwaka huo ndio ambao niliendelea kufungua macho zaidi na kuona mengi sana. Ni mwaka huo niliujitukia kwamba napenda tamasha za maziki, niliudhuria tamasha hizo nyakati nyingi sana na ziliniifurahisha. Nilipokuwa darasa la tano (5) hali ilizidi kuwa nzuri na hapa ndipo nilipogutukia Masomo na nilifitahidi sana na makumbuka niliwali kuwa wa tatu kwa mkwala wa kwanza, nafasi ya nane kwa mkwala wa pili, na nafasi ya tano kwa mkwala wa tatu, hata hivyo sikukata tamaa ya kushika nafasi ya kwanza.

Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na moja nikazidi kuwa na akili ya kilimo, Wakubwa zangu wali-nifunza jinsi ya kulima mahindi, pojo, kunde, matoragwe, mpunga, hata jinsi ya kukata ngomba na jinsi ya kukata mkungu wenyewe. Kazi hizi zote nazipenda lakini mahindi na mpunga humikasirisha sana. Hii ni kwa sababu ya tumahitaji au inahitajika kulinda ndege, mayoneta*, nguruwe, na panya. Kwanza kabisa nilazungumzia na kuchora jinsi gani wanayama kwa wauamichukiza.

* → Ukiada mwingine → *



Ukiona ndege sasa inakubidi uwafukuze kwani wakiingia shambani kutatamani au kutumana kupata mpunga hasa kumbinda ndege mimi sipendi, hata linyo wakati wa kula chakula sivuzi kusema sipendi, nitakwambia ningoje nye mnywe maji hali mimi ninakula mpunga, wewe unakaa nje.

Hata linyo singechoka kutoa mfaano mwingine. mahindi.



Mahindi maysi yanahitaji kupalilwa kwani bila kupalilwa hwa hufa na kupata mazao yoyote, hii ni mngawapo wa kazi ambayo nimechukia. Baada ya cyte kuma na kazi moja ambayo vilevile ni ngumu, maysi ni kuvuna kwa kupata mpunga ni uzingatia nje zifuatazo


Kuweka mpunga nda ya shamba → kutia maji shambani
 → kupalilwa shamba → kupanda mpunga kwenye nafasi
 → kulinda mpunga → hukata mpunga → kupileka mpunga
 au.

(3)

Mahindi

- ① Kupanda mahindi au kuvetsa mbege kwa mchanga.
- ② Mbege zinachipuka na kutoa miti wa hundi.
- ③ Kupatia nyasi kwonye shamba.
- ④ Kuangalia mimea isichambiwe na majonda.
- ⑤ Kuvuma
- ⑥ Kuchepesha mazao nyumbani.

Singependelea sana kuongeza bali ukirangabika mwenyewe ni njia ndiye na tunapata slides sana lala hivyo tumeroka kulima. Ningependa pia kueliza habari kidogo kuhusu migomba au ndizi kwani pia tunalima ndizi kwa wingi sana. Ningependa pia kuchora mgomba pia-



(4)

Maneno Magumu	Hwa upande wa migomba hatupati taabu kwani
1 tumesinywa	migomba iki kama km mbili na nusu hivi kutoka
2	kwa mji, hata hivyo si kwamba hatupati hasara
3	hasara tunafuta kwani kuna wanyama wa ponzi
4	kama vile nyati, ndovu nguruwe n.k. Hawa ni baadhi
5	ya wanyama ambao hutia hasara kwa mpunga na
6	pia mahindi, hata na migomba pia.
7	Kwa hasara tunazopata ni kwamba
8	kwanza kabisa nyati akiingia kwa migomba hasara
9	yake ni kuvunja vinya mimea yote ile anayopikula
10	mpaka atakapotoshika ndipo huachana na hiyo mimea.
	Ni hasara kwa mwenye shamba kwani itambidi angayo
	msimu mwingine ili apate ndizi.
	Ikiingibia nguruwe naye ana hasara kwani
	unapata kwamba yeye hutaka kupata ile mkungu
	wenyewe na ahakula na kuvunja. Hii ni hasara
	kwani pengisi mwenye shamba alitorajia kutumia
	mkungu huo kwa siku hiyo lakini kwa vile
	unelwa na nguruwe itambidi hutafuta mwingine
	wa kuwa anaweza kukata.
Majibu	
1 hatupendezi	Hata hivyo sisi wanamashamba hatupendezi
2	au tumesinywa na mnyama huyu; Ndovu ama
3	kwele yeye ni mnyama hatari, mpole pia lakini
4	ana tabia mbaya kwani yeye hutuma migomba
5	kama mwa yake na hiyo; sisi wakulima kwa jumla
6	tunachosikwa sana na tabia ya mnyama huyu na
7	hatupendi sana. Hukata mmoja haumei tena
8	sinependa kueleza sana ambapo nachani hivi yatosha
9	kukusiana na migomba.
10	Tunapenda sana sisi wapokimo kuanda kustika
	samaki mtoni, ziwani, au hata kwa maziwa madogo.
	Hali hii pia ni mojawapo ya masha yetu jinsi ile


(5)

sisi wapokomo tunaishi, kwa kuanzish, ningesema kwamba tunapenda samaki sana na ni majawapo ya vyakula yetu tuvipendayo. Kwa kweli tuna aina tatu za samaki pia na aina nyingine ambazo ni nne kwa jumla. Kwanza tuna (Kamongo) → kiswahili (Mud-fish) → kiingereza. Aina hii ya samaki ndiyo watu wengi wanaipenda sana na hata waingerereza ndakaja hula samaki hiyo. Pili tuna (Mtonzi) → kiswahili (Mud-fish) kiingereza kwa kweli samaki za aina hii zina mero mmoja na huanza ukitia kidole ndani ya melomo wala, hata hivyo sisi hutumia kwa mboga yetu.

Tatu tuna (Parapara) → kiswahili (Tilapia) Aina hii lupatikana sana kwenye maziwa na ina miba mingi sana. Kikaranga hata hivyo huwa ni towa zaidi na tunaipendelea sana. Hata hivyo sisi hutumia vifaa kwa kuanzish samaki, mara nyingi tunatumia Ukongo na mikuti kwa kudungia samaki, pia tunatumia mishipi lakini si sacana, wya ilizi zote zinatumika mahali pamoja kwani hutumia zote utafanua lupata samaki.

Mto ambao tunapenda kugolea ni mto Tano ambao ni mpama sana pia maziwa ni kwa mfaano: Chamaadho, Jange, Kibwala cha Mjeko, Giritu nk. Haya ni majina ya lipokomo ambayo kila jina lina maana ya kute fulani, siamaliza babu yangu maana yake kwani sijafika umi wa kujua maana yake. Kwa hivyo ninasahiza kueleza kuhusu samaki na mto nk kwa kusema tunajitahidi sana kwa ndiyo mboga ya hula.

Kwa upande wa familia yetu sisi na ukoo wetu kabila letu sisi ni (Wasalanchini) Thomas anafahamu vizuri na tuwajokomo rilevile.



(6)

Sama pale kijijini, au wangi pale kijijini ni WAKAFOLIKI na hata mimi ni mmoja wao tuna huchuria ibada siku ya ijuma kwa vijana saa moja asubuhi, Jumamosi ni siku ya maungano na tunaanza misa yetu au ibada ni saa mbili na saafiki

Kufika hapo nadhani nimetoa kuwifa ya kutosha kuhusiana na maisha ya kijiji chetu na jinsi ili tunavyoishi upande wa chakula.

Hivi sasa nasoma darasa la nani (8) kuko Ruben Mwewe Boarding school na mwaka huu wa 1988 mwalimu wangu mkuu Mr. TOLA N. DABDAH alinichagua kuwa head prefect tarehe 8 Januari nami nilidifurahi na nazihi kufurahi kwani ninazidi kuwa na ujuzi wa kusimamia mambo makubwa. Mwaka huu wa '88 mwezi wa Agosti tarehe (12) Ndipo huli yangu ilibadilika, sikawa nikikuathiria masomo ya kujisomea vizuri, nilikuwa mgongwa

Nilionda kwa Dispensary ya mission na walinambiwa ninahitaji X-ray kwani roho yangu ilikuwa haijigaji vizuri. Basi nikazidi kuwumilia na shule zikafunguliwa, lakini sikuwaza kusoma vizuri ilinibidi mionde kwa linyo X-ray Mombasa, ilikuwa hivi, nikiondoka nyumbani nitafika Malindi nishukie EDEN ROCK HOTEL nimpate ndugu yangu, anipetaka mombasa. Nilifanya linyo na nikiondoka nyumbani sasa huni na moja na kufika malindi saa moja. Nilikuwa mgani na kwa linyo ilinibidi nitafute hoteli Eden Rock, nilifaulu mwisho na nitamaliza ndugu yangu lakini hikaambiwa amekwenola Mombasa kwa leave yake, sasa nilifikiria sana Niende Mombasa msikokupus au nikaidi I/River? Nikaamua kuwonda kwa river, hata linyo sikuwaza na nauli ya



Murudia J. Diver. Katika hali ya kutafutsa msadala nitikuwakiwa kumpata mjerumani mmoja wa kike kwe jina Anne Schwarz na aliwasaidia na nauli pia alinipa chakula cha mchana kwani nitikuwa sijapata chakula. Tukzungumza sana na ilifika saa nane mchana na ikambidi kwenda stage ili wipate Basi ya saa tisa. Nim ni mtu wa Bahati mbaya sana kwani nitipokwenda, ilikuwa imekwisha ondoke kitambo, shida nyingine ilinikabili, sikwa na mahali pa kulala. Nilisumbuka sana kutafuta mwishowe niliamua kumuona Anne Schwarz katika Lutheran Guest House Malindi.

Ilikuwa saa moja na maolakika na bahati niliruhusiwa kwenda kumuona, Alikuja, tukasalimiana na nikamueleza shida chiyonikabili naye akaniambia nimsubiri, Punde akaja na mtu mwingine mkelewa mwape upana wa kadiri na mrefu, Nilimwleza mtu huyu shida yangu, kwamba alinuliza jina, mahali ninapoitishi nami nikamjibu, Aliziidi kumitajabisha kwa kumsalimia kipskomo. Sikusita nilimjibu na akanijulisha jina la ke kama Thomas Greider na kwamba alifahamana na Babu zangu hino Joseph Mbizi, Eustus Buko Erastus Buko nami nilifurahi kwamba aliwafahamu.

Nitilalika kwa chakula cha jioni nami nititi tumis na luku tuwongea, Walinieleza kwamba was ni wajerumani ishirini waliokuya kuyifuma kiswalia na kwamba watarudi kawao baada ya witi mbili. Waliniandakiza mahali pa malazi chumba nembavi 4 nikalala hadi asubuhi.

